# *Magonjwa Na Mateso*

Ninataka kuelezea jambo fulani, baadhi ya mambo muhimu ambayo mnapaswa kujua. Sauti yangu si kubwa sana, kwa hivyo labda itabidi nifike *hapa*. Bwana akiruhusu, Jumapili alasiri, ninataka kuzungumza nanyi katika mahubiri ya Injili ya kiinjilisti, Jumapili alasiri. Nasi tunatarajia mambo makuu, Bwana kututendea juma hili.

2 Jambo moja linahusu. . .wengi hapa wangeshindwa kuelewa jinsi hizi kadi za maombi zinavyo—zinavyotolewa kwa wagonjwa na wanaoteseka. Katika miaka mitatu ya kujaribu, huu ndio mpangilio pekee ambao nimewahi kupata ambao ilionekana kwamba ulikuwa umebarikiwa na Mungu.

3 Kwanza tungeingia tu na hatuna kadi hata moja, na kuwaacha tu watu wapange mstari. Ilikuwa ni msongamano mkubwa sana, pia. Ndipo ningepata kuomba labda dakika kumi na tano, ishirini kwa wakati mmoja; umati ungenifikia, na ingewalazimu kunitoa nje.

4 Na halafu lililofuata, likaanza, tungetuma kadi za maombi kimbele kwa wahudumu. Na kila mhudumu akifadhili, labda makanisa hamsini au zaidi katika eneo lote yangefadhili mkutano, na kila mhudumu angekuwa na kadi zisizopungua mia moja. Kila mhudumu alitaka kusanyiko lake kwanza. Angewapa kusanyiko lake na pengine siku zote nne au tano usiku, kusanyiko la mhudumu mmoja tu lingeingia, hao wengine wangejisikia vibaya sana juu yake.

5 Kisha tukafikiria kuwa na wenyeji, wenyeji tu katika jamii; na wakati mwingine watu huja maili nyingi kama elfu saba, nane kwenye mikutano. Hiyo haikuwa sawa.

6 Na njia pekee ambayo tuliona kwamba tunaweza kuwa, kweli kumwacha Bwana atengeneze njia, ni kuja na kuchukua kadi za maombi, kama hamsini hivi, na kuzitoa tu kwa makundi ya watu, wala hakuna ajuaye ni nani atakayeingia.

7 Niliona wakati nilipotoa kadi hamsini na hakuna hata moja ya hizo kuitwa. Ninaanza kwenye mkutano, na Roho wa Bwana ananiongoza moja kwa moja kati ya watu, namna hiyo, kamwe nisitumie hata kadi za maombi.

8 Niliona wakati ambapo ningeketi jukwaani, na kuanza tu kuzungumza, na ninajisahau tu kabisa kwa saa moja au zaidi, muda, wakati nikimwita wa kwanza, na kisha mwingine namna hiyo. Ninge. . .Kila mmoja aliponywa.

9 Watu wengi hukusanyika kwa ajili ya m—mstari basi. Nilitoa tamshi hili, ni kweli, limekuwa zuri kwa miaka mitano. . . kwa miaka mitatu sasa. Samahani. Kila mtu anayekuja

kwenye jukwaa hili ameponywa. Hakujawa na kitu chochote, haijalishi kilikuwa kimepotoshwa vibaya kiasi gani, kilema, au anayeteseka, daima kinaponywa. Kumekuwa na visa vya kutisha. Lakini mimi . . . Labda, kwa wakati wa usiku mmoja, ningeweza tu kupata labda tatu au nne au tano. Labda wakati mwingine . . .

10 Niliona wakati mmoja kule Calgary, Canada, walipata mbili tu, ambapo watu ishirini na tano elfu walikuwa wamekusanyika. Mbili.

11 Mmoja alikuwa mvulana aliyekuwa ameteseka kwa muda wa miaka kumi na minane, mkono wake ulikunjamana chini yake. Alikuwa kwenye kiti cha magurudumu. Mama yake alikuwa ameweka pete yake ya harusi rehani, ili kumtunza. Aliishakuwa katika mikutano saba au minane hivi; kamwe hakuweza kupata kadi. Hatimaye wakati wake wa kuwa jukwaani ulifika. Mvulana akatoka kwenye jukwaa. Asubuhi iliyofuata, alijinyoa kwa mara ya kwanza maishani mwake. Akakutana nami huko nje kwenye njia panda ndege iliposhuka Vancouver, kunipa mkono.

12 Msichana mdogo ndiye aliyefuata. Msichana mdogo, Mkatoliki kwa imani, mguu mmoja ulikuwa mfupi kwa inchi nne kuliko mwingine. Tulikuwa na kama saa moja na kitu na msichana huyo mdogo. Na Biblia ii hii . . . Walipomleta pale, angeshuka chini pembeni. Niliiweka Biblia hii kichwani mwake, alitembea kawaida tu kama mtoto yeyote, huku na huko kuvuka jukwaa, wakati wale watu elfu ishirini na tano wameketi, wakitazama. Lakini, mambo hayo, tunasema tu.

13 Sijui mtu yeyote humu ndani aliye na kadi ya maombi, ama ni nani atakuwa wa kwanza. Tunatoa kadi hizo na kisha tunaingia.

14 Nitajaribu na kukupa wazo. Ndugu yangu anasema, "Nilitoa kadi hamsini."

15 Nikija kwenye jengo, huenda nikakutana na mtoto mdogo. Ningesema, "Je, unaweza kuhesabu?"

Anasema, "Naam, bwana."

Ninasema, "Anza kuhesabu."

16 Labda angehesabu hadi kumi, kumi na tano au ishirini, na kuacha; popote aliposimama, ningeanzisha mstari wa maombi. Kama angesimama kwenye ishirini, ningeanza safu ya maombi kwenye ishirini, na labda kwenda mbele au nyuma.

17 Labda usiku uliofuata ningehesabu watu wengi kwenye safu na kugawa mara mbili, na kuona ni nambari gani, ama kitu kama hicho.

18 Hakuna ajuaye bado, usiku wa leo, mahali ambapo mstari wa maombi utaanzia; popote tu inapoonekana sawa. Wakati

mwingine huangukia moja kwa moja kati ya vilema. Wakati mwingine huangukia kati ya wagonjwa. Sijui. Hakuna anayejua. Tunatoa tu kadi na kumwacha Bwana aongoze kwa yale yaliyosalia, na daima imefanya kazi vizuri kwa njia hiyo. Iweni katika maombi.

19 Ninaamini haya yote ni mapya kwenu watu hapa. Katika mikutano yote ambayo nimewahi kuwa, huu ndio mkutano mdogo zaidi wa usiku wa pili niliowahi kuwa nao kwenye mkutano wowote tangu niingie hudumani. Kwa kawaida, usiku wa pili, ukumbi wowote, au kutangazwa kwa njia yoyote, kwa kawaida hufikia elfu saba, nane, kumi, kufikia usiku wa pili. Bila shaka, imetangazwa tu mahali hapa. Kinacholeta umati huo, kwa sababu unatangazwa kimataifa, na mamia mengi hutoka jimbo moja, na majimbo mengine, kufanya kundi hilo.

20 Mkutano wangu unaofuata baada ya hapa utakuwa Houston, kwenye ukumbi wa michezo. Nafikiri unaketi watu elfu kumi na saba, nadhani. Tayari uko kwenye magazeti manne au matano ya kimataifa. Hapo ndipo watu hutoka, kuvuka bahari na kadhalika, kila mahali.

21 Ningependa kusoma kidogo tu Neno usiku wa leo, kwa maana Neno la Mungu halishindwi kamwe. Maneno yangu yatashindwa; Neno Lake halitashindwa. Inapatikana katika Zaburi 103, kifungu cha kwanza, cha pili, na cha 3.

> *Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana: naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu.*
>
> *Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, wala usizisahau fadhili zake zote:*
>
> *Akusameheaye maovu yako yote; akuponyaye magonjwa yako yote;*

22 Mungu na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake! Haya yote, nikizungumza juu ya *Magonjwa Na Mateso*, ningependa kwa dakika chache tu nitoe matamshi kadhaa kuyahusu. Nami nawatakeni msikilize na myape usikivu wenu mkamilifu.

23 Magonjwa na mateso yote ni matokeo ya dhambi, labda si katika maisha yako, lakini katika maisha ya mtu kabla yako. Ibilisi ndiye mwanzilishi wa magonjwa na mateso. Kabla hatujawa na ibilisi, hatukuwa na magonjwa wala mateso. Lakini, Shetani alipokuja, alileta magonjwa na mateso pamoja naye.

24 Kuna nyakati nyingi sana ambazo tunazitaja kuwa baraka. Siwezi kamwe kufikiria kwamba Mungu angeweza kupata kuhimidiwa kutoka kwa mtu mgonjwa; isipokuwa awe ni mwenye dhambi, ukimpeleka kwa Mungu; au mtoto asiyetii, kumrudisha ili apatanishwe na Baba yake. Lakini magonjwa ni matokeo ya ibilisi na kule kuanguka. Hapo . . .

25 Leo, tuna madaktari bora zaidi ambao tumewahi kuwa nao. Tuna sayansi bora zaidi ya matibabu, hospitali bora zaidi ambazo tumewahi kuwa nazo; na magonjwa mengi kuliko tuliyowahi kuwa nayo. Na katika siku ambayo tumepata sayansi bora zaidi ya matibabu ambayo tumewahi kuwa nayo, daima wanajenga taasisi kwa ajili ya wasioweza kupona. Papo hapo tulipo na kazi bora zaidi ya kisayansi juu ya mateso na magonjwa tuliyopata kuwa nayo; kujenga taasisi, kila mwaka, kwa ajili ya magonjwa yasiyotibika.

26 Lakini hakukuwa na kitu chochote kilichokuja mbele za Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ila kile alichokishinda kwa mbali. Na Yeye ni yule yule tu leo kama alivyokuwa jana, na atakuwa hata milele. Naye anathibitisha hilo. Na utaiona, usiku baada ya usiku. Na kama sivyo, basi una haki ya kutilia shaka.

Mtu fulani alisema, “Je, uponyaji hudumu?”

27 Unadumu kadiri imani inavyodumu. Lakini imani inaposhindwa, basi uponyaji wako utashindwa. Je, unaweza kusema kila mtu aliyekuja madhabahuni na kuongoka angekuwa Mkristo siku zake zote? Anaweza kuwa usiku wa leo mtoto wa Mungu, na kesho akawa mtoto wa ibilisi. Ni wakati anapopoteza imani kwa Mungu, ndiyo inamrudisha nyuma.

28 Na nguvu zozote zinazoweza kukuponya hapa kwenye jukwaa hili zinaweza kukudumisha mzima. Hiyo ndiyo sababu nilitoa kauli hii, ya kwamba, hakuna kitu kinachokuja hapa ila kile kinachotolewa hapa. Hapa nje, ni kulingana na imani yako kama inadumu.

29 Nimeona watu wakija jukwaani, vipofu kabisa, na kusoma Biblia ii hii. Chini ya siku tano, wanarudi tena vipofu kama walivyowahi kuwa. Kwa nini walisoma hapa? Nguvu za shetani zilitambua kipawa hicho cha Mungu na ikabidi aondoke. Sasa hiyo ni mb-. . .hiyo ni. . .Najua hilo ni tamshi kwelikweli kutoa, lakini najua ninaposimama. Nami ninajua ambaye nimemwamini, na ninajua nguvu Zake za kuponya.

30 Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita nilipokuwa Phoenix. Mistari ya maombi ilikuwa imefika mbali mitaani; hawakuweza hata kuingia kwenye ukumbi. Kuingia kwenye mstari, mtu fulani alisema, “Hivi—hivi huogopi, Ndugu Branham, kusimama hapo mbele ya mambo hayo yote na kutambua kwamba wakosoaji wamesimama hapo na waandishi wa magazeti, na kadhalika, kukosoa?”

31 Nilisema, “Siogopi mradi tu ninahisi kuwa Yuko karibu. Lakini kama siwezi kumhisi, ningetoka jukwaani na kwenda nyumbani.”

Hakuna mwanadamu anayeweza kufanya lolote. Yote hayana budi kutoka kwa Mungu.

32 Kwa mfano, tutachukua. . .kuzungumza kwa muda mfupi kuhusu kansa. Inaonekana kuwa mmoja wa maadui wakuu leo. Kansa ni nini? Ilitoka wapi? Uvimbe, mtoto wa jicho, kidonda, nimonia, kifua kikuu, majina yote hayo ni majina ya matibabu ambayo sayansi ya matibabu iliyapa. Biblia inayatangaza kuwa ni mashetani. Kwa mfano, kansa, kansa ni nini? Kawaida hutoka kwa mchubuko.

33 Mambo yote ya asili ya dunia ni mfano wa kiroho. Kila kitu katika asili hufananisha cha kiroho. Mnajua hilo, wengi wenu.

34 Kwa mfano, kama vile mtoto anapozaliwa, na mtoto anapozaliwa na Mungu. Wakati mtoto, wakati mtoto anapozaliwa katika Ufalme wa Mungu. . .Biblia ilisema, "Kuna watatu wanaoshuhudia Mbinguni, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu."

35 [Mtu alilia mara kadhaa—Mh.] Sasa, ni mtu fulani ni mgonjwa ama kitu fulani, kwa hiyo nipeni tu usikivu wenu. Ukikosa mambo haya, pengine utakosa uponyaji wako, kabisa.

36 "Wapo watatu wanaoshuhudia mbinguni." Sasa, wakati sisi. . .Uongofu wetu. Kitu hiki kilitoka kwa mwili wa Yesu Kristo alipokufa; kulikuwa na maji, Damu, na Roho, na vitu hivi vitatu vinafanyiza Kuzaliwa upya. Hiyo ni kweli, wahudumu? Vitu hivi vitatu vinafanyiza Kuzaliwa upya; maji, Damu, na Roho.

37 Hivyo hufanya kuzaliwa kwa kawaida, wakati mtoto anapozaliwa. Kitu cha kwanza ni nini? Maji, damu, uhai. Mambo yote ya asili ni mfano wa ya kiroho.

38 Na kansa, katika asili. . .Katika kiroho, yeye ni ibilisi.

Yeye hufananisha mla mizoga na mwewe; anakula vitu vilivyokufa.

39 Kansa inatokana na mchubuko. Kwa mfano, mkono wangu, ha—ha—hauna kansa yoyote juu yake. Na unaweza kuwa nayo, wakati fulani. Vema, ni nini husababisha kansa? Hivi. . . Seli fulani, chembechembe mwilini mwangu, inarudi nyuma, inapondeka, ama kitu fulani kinaingia. Na kutoka kwa chembechembe hiyo, au seli, huanza kuzidisha seli, kuzidisha, na inatengeneza kansa na inaanza kula kuingia mwilini.

40 Sasa, kila uhai, na kila chembe ya uhai iliyopo, ilikuja. . . hutoka kwa seli. Wewe mwenyewe ni kutoka kwa seli ya uhai. Ulikuja, wakati mmoja, ulikuwa ni seli ndogo tu, ndogo kabisa haingeweza kuonekana kwa jicho la kawaida. Ulitoka kwa baba yako. Wewe si kitu, hakuna damu ya mama yako hata kidogo. Seli ya damu hutoka kwa jinsia ya kiume. Na halafu kutoka kwa seli hiyo, inakuwa kuzidishwa seli. Na kila kitu kwa jinsi yake; seli kutoka kwa mbwa itazaa mbwa, kutoka kwa ndege ndege, mwanadamu mwanadamu. Kama hakuna kitu kitakachokatiza huo, mpango wa Mungu, hakuna kinachoukatiza, utazaa mtoto

mkamilifu, wa kawaida. Na atakua na kuwa mtu mzima mkamilifu, wa kawaida, ikiwa hakuna kitakachoukatiza. Lakini kitu kinapokatiza, basi ni lazima iwe ni uovu unaokatiza mpango wa Mungu.

41 Mungu hakukusudia uwe mgonjwa. Mungu alikuumba kwa sura Yake. Anataka uwe mzima. Amefanya kila awezalo kukuweka mzima.

42 Naye Shetani yuko dhidi yenu. Kwa hiyo, kansa hii yeye—yeye anaanza, ama uvimbe huu, chochote kile, kutoka kwa vijidudu huanza kuongezeka, kama vile uvimbe unavyokuwa mbaya, kadhalika. Ni mwili, kama vile tu wewe ni wa mwili. Ina roho kama vile wewe ni roho, ila tu haina nafsi. Lakini ina uhai kama vile ulivyo na uhai. Na kwa hiyo, basi, ndani yako, katika mwili wako, kuna maisha mawili. Mmoja ni wewe na mwingine ni kiumbe kingine, kikizidisha seli, kukuza mwili, kama vile ulivyokua katika mwili. Je, hiyo ni kweli?

43 Naam, basi, ni nini inafanya hiyo? Ibilisi. Ki—kijidudu ni uhai. Kwanza, kijidudu ni seli ndogo yenye uhai ndani yake. Na uhai huo unaweza tu kutoka kwa rasilimali mbili, ama kutoka kwa Mungu au shetani. Nawe ulitoka kwa chembechembe ya uhai, kwa njia ya Mungu. Kansa, uvimbe, ama kadhalika, hutoka kwa chembechembe ya uhai kwa ibilisi. Na anajaribu kuharibu maisha yako. Anakula mkondo wa damu yako na—na njia tofauti anazofanyia kazi juu yako. Kwa hiyo, najua kwamba wao ni mashetani. Yesu Kristo aliwaita mashetani. Na anachosema Yeye ni Kweli. Wao ni ibilisi. Ibilisi ni mtesi. Yuko hapa ili aurarue mwili wako, akule wewe, akuangamize, afupishe "sabini yako," kama anaweza.

44 Hiyo ndiyo sababu Malaika huyu wa Mungu anaposhuka hadi nilipo. . . Sijui chochote kuhusu yeyote kati yenu. Lakini hiyo ndiyo sababu anakuambia aina ya ugonjwa ulio nao mwilini mwako, kwa sababu kwamba uhai huo uko chini ya Uhai ambao Mungu aliteremsha ili kuupambanua. Na kisha mambo ambayo umefanya katika maisha yako. Inafanywa kwa uwezo wa Mungu, basi ninaweza kujua kama iko pale au kama imetoweka. Na unaweza kuiona kwa matokeo ya kimwili yaliyoonyeshwa. Unaweza kumwona mgonjwa, wakati mwili wake unakuwa sawa na wa kawaida, macho yake yanafunguka, au masikio yake yanafunguka.

45 Sasa ni nini? Unasema mtu, kama mvulana mdogo hapa, ama ninaamini baadhi yenu walikuwa huko maskanini siku chache zilizopita usiku kuona. Hii hapa picha ya mahali ambapo *Chicago Tribune* ilitoa, ya bubu tisa, ambao waliwapeleka huko, waliotoka katika taasisi hiyo, waliozaliwa viziwi na bubu, mmoja wao kiziwi, bubu na kipofu. Sasa labda baadhi ya wasimamizi wamekusomea maelezo hayo. Sasa watu hao, magazeti kama *Chicago Tribune,* si washupavu. Kesi hizo

zinapaswa kuchunguzwa kikamilifu kabla ya kuwekwa kwenye gazeti kama hilo, la *Waukegan Sun,* au *Post Dispatch,* au lolote la magazeti hayo. Sio ushupavu. Si kuchochewa, imani bandia, au nadharia. Ni Nguvu za Mwenyezi Mungu. Na Yeye yuko hapa kuithibitisha usiku wa leo, na ataithibitisha. Na haraka kadri wasikilizaji wetu wanavyokuwa na nia moja na moyo mmoja . . .

46 Kama hili—kama kundi hili la watu linaloketi hapa, labda lile litakaloombewa usiku wa leo, kuja jukwaani, ikiwa watakuwa katika moyo mmoja na nia moja; katika dakika tano tu zijazo, hakutakuwa na mmoja wao kwenye viti hivi vya magurudumu au vitanda. Kama wataamini ya kwamba hii ni Kweli. Na wanapokuja, mmoja mmoja, usiku wa leo, jukwaani; kama wao, kila mmoja, hawajachukuliwa kutoka kwenye hivyo viti vya magurudumu na vitanda na kadhalika, na kuondoka kwenye jukwaa hili, wazima, basi unaweza kusema nimekosea.

47 Nami narejea kwa Mungu, Ambaye, Yeye hakosei. Utapona. Sasa Yeye yuko hapa kulitimiza Neno Lake. Kila Neno analosema Mungu ni kweli. Lakini hupaswi kuliamini nusu nusu; huna budi kulijua.

48 Watu wengine wanakuja, wanasema, "Naamini." Wanafikiri wanaamini; lakini kama ungepata mmoja kati ya kila elfu moja anayeamini kweli. "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."

49 Tunatawaliwa, miili yetu inatawaliwa, na hisi tano. Ni wangapi wanaojua hilo kuwa kweli? Hebu tuone mkono wako. Hisi tano; kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Hiyo inamtawala mwanadamu wa asili.

50 Sasa kuna mtu mwingine ndani, ambaye ni mtu wa imani, roho. Ana hisi mbili. Moja yazo ni imani, hiyo nyingine ni kutokuamini. Ambayo, hufanya idadi kamili ya Mungu, saba, hisi ulizo nazo.

51 Sasa, karibu yeyote wenu hapa ndani bila shaka angeapa kwa hisi zako tano. Sasa angalia hili kwa muda kidogo.

52 Je, unaweza kusimama hapa, kwa muda kidogo tu, Dk. Cauble? Sasa ninaamini kwamba kuna mtu aliyesimama mbele yangu, amevaa suti ndogo yenye mirabamiraba, amevaa miwani, na tai nyekundu. Ni wangapi wanafikiri niko sawa, hebu tuone mkono wako? Vema, unajuaje kuwa kuna mwanamume aliyesimama pale? Kwa sababu unamwona. Je, hiyo ni kweli? Sasa hiyo ndiyo njia pekee, hisi pekee, niliyo nayo sasa ingeniambia kuna mtu aliyesimama pale, kwa sababu ninamwona. Kuona kunamtangaza.

53 Vema, simwoni sasa, lakini bado ninaamini yuko. Sasa unasema, "Kuona ni kuamini." Ndivyo? Ninaamini kwamba Dk. Cauble amesimama pale sasa, na simwoni. Kwa sababu, nina hisi ya mtu binafsi, mbali na kuona; inaitwa kugusa, na ninahisi

yuko hapo. Na najua ni Dk. Cauble. Si Dk. Bosworth. Maana, Dk. Cauble alikuwa na Agano dogo mkononi mwake, nalo bado lipo. Kwa hiyo mimi . . .?. . . Nilitoa tamshi hilo wakati mmoja na mtu akanipenyezea mtu mwingine kisiri. Lakini niliona ya kwamba Dk. Cauble alikuwa na Biblia hii ndogo mkononi mwake, na ni Dk. Cauble. Sasa njia pekee ambayo ningeweza kujua kwamba alikuwa amesimama pale sasa ni kwa hisi ya kugusa. Nami ninajua ni kweli.

54 Lakini sasa simgusi hata kidogo. Hisi hiyo imekufa kwangu, lakini najua yuko kwa sababu ninamwona. Unaona ninachomaanisha?

55 Kuna hisi mbili tofauti za mwili zinazosema kwamba yuko hapo. Mojawapo, namwona. Inayofuata, ninamgusa. Sasa kunatokea . . .

Simama tu hapo kwa dakika moja, ndugu.

56 Sasa nina hisi nyingine, nayo ni ya kusikia. Piga muziki wa kitu fulani. [Mpiga kinanda anaanza kupiga—Mh.] Ni wangapi wanaoamini kuwa kuna muziki unaopigwa? Hebu tuone mkono wako. Je, unauona? Je, ni wangapi wanauona huo muziki? Je, unaunusa, unauonja, unaugusa? Naam, unajuaje kuwa ni muziki? Umepagawa . . . Vipi ikiwa mtu hakuwa na hi—hisi hii ya kusikia sasa hapa ndani? Hawangejua kuwa muziki unapigwa; hisi hiyo imekufa kwao. Hawangeweza kuusikia, kwa sababu hawawezi kusikia. Lakini wewe ambaye una hisi ya kusikia unajua unapigwa kwa sababu unausikia. Huwezi kuuona, huwezi kuuhisi, huwezi kuunusa, huwezi kuuonja, lakini unaweza kuusikia.

57 Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo usiyoyaona, kuonja, kugusa, kunusa, wala kuyasikia. Lakini hisi ya imani ni halisi kama vile kuona kwako kulivyo, ama yoyote ya hisi zako. Unaona ninachomaanisha? Unaamini, wewe ninii tu . . . Hakuna mtu anayeweza kukufanya uitilie shaka, kwa sababu unayo hiyo hisi inayokuambia ndivyo hivyo.

58 Ungesema, "Shati hilo lilikuwa jeupe." Vipi kama ningekuambia lilikuwa jekundu? Vema, huwezi kuamini, kwa sababu ni jeupe. Hisi yako ya kuona inasema ni jeupe. Macho yako yanasema hivyo.

59 Vema, sasa kama unaamini, wewe hapa wa kuombewa, yeyote uliye, kama unaamini usiku wa leo kwamba utaponywa, kwa dhati tu kama vile macho yako yanavyosema kwamba shati hilo ni jeupe, kazi imefanywa sasa hivi.

Asante, Dk. Cauble.

60 Hiyo ni kweli. Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo usiyoyaona, kuonja, kugusa,

kunusa, wala kuyasikia. Ni hisi nyingine. Iko katika ulimwengu mwingine. Si kitu cha asili.

61 Huwezi kupata chochote kutoka kwa Mungu, isipokuwa kwa imani. Kwa imani kuta za Yeriko zilianguka. Kwa imani Musa alikataa kuitwa mwana wa binti Farao. Kwa imani Gideoni alifanya hivi na hivi. Kwa imani, njia pekee!

62 "Na pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu." Na ukitaka kumpendeza, ni lazima uje Kwake kwa imani, ukiamini Neno Lake ni Kweli.

63 Kwa nini ninasimama na kutoa tamko hili la maneno na kusema kwamba hakuna kitu kinachoweza kuja kwenye jukwaa hili bila kutambuliwa na kutaja magonjwa, siri za mioyo? Na haijalishi amelemaa kiasi gani, hakuna mtu, ambaye amekuwa katika mikutano mingine, ila anayefahamu ya kwamba kila wakati wanaponywa. Kwa nini? Malaika alipokutana nami, alisema, "Ikiwa utawafanya watu wawe waaminifu..." Au, "Kama utakuwa mwaminifu na kuwafanya watu wakuamini, hakuna kitakachosimama mbele ya maombi yako." Ninaiamini. Na kama ninaweza kukufanya ufanye jambo lile lile; Louisville, Kentucky kutakuwa na mtikiso ambao haujawahi kutokea hapo awali. Hiyo ni changamoto.

64 Lakini ninachojaribu kufanya, usiku wa leo, ni—ni kukufanya uone ninachomaanisha. Ndipo unapokuja hapa, na kukombolewa, simama moja kwa moja kwenye Neno hilo. Yeye—Yeye ndiye Kuhani Mkuu wa maungamo yako. Mungu hawezi kukufanyia lolote mpaka kwanza ukiri kwamba Yeye yuko. Ndipo unapolikiri, basi liamini, litendee kazi na ukae nalo, na Mungu atakutoa. Je, unaamini hilo? Kweli.

Hapa si muda mrefu uliopita huko Fort Wayne, Indiana...

65 Pamoja na hayo, nina taarifa ndogo pale, Dk. Bosworth, kwenye mfuko wangu wa kabuti, watakuletea, ya m—mkutano tuliotoka hivi punde, katika *We The People*. Ninaamini ilikuwa ni msichana mdogo kipofu, ambaye waliichapisha. Itakuja katika *We The People* sasa, kitabu kinachoenea ulimwenguni kote, mwandishi wa gazeti aliyeandika taarifa ya kukosoa, alisema, "Msichana alidai kwamba alikuwa ameponywa, na hakuwa." Naye maskini msichana huyo ana maelezo ya daktari, na kadhalika namna hiyo, na kuichapisha. Na kisha wakaichunguza, na sasa imeenda kwa *We The People*. Mungu atafanya kazi, na hakuna awezaye...Nitamruhusu Dk. Bosworth awasomee, labda, katika ibada ya kesho alasiri. Imetumwa tu na gazeti la Fort Wayne huko juu.

66 Bibi Bosworth, katika mkutano; walikuwa wakiendelea, baadhi yao walikuwa wakisema...Kulikuwa na mtu ameketi pale mwenye ugonjwa wa kukacha kwa misuli, amepooza kwa miaka kumi. Naye alikuwa na ugonjwa wa kupooza wa kutambaa, ukaingia kwenye uti wa mgongo wake. Alikuwa

mfanyabiashara wa mjini. Na hawakujua. . . Walikuwa wamemketisha pale. Na walikuwa wamewaona wengi kwenye viti vya magurudumu, na watu wanaoteseka, wakikombolewa. Basi usiku huo, msichana mdogo mwenye makengeza nyuma ya jengo alikuwa ameona watu wengi wakikombolewa, wenye makengeza.

67 Sijawahi kuona mtoto yeyote aliye na makengeza akija jukwaani ila aliyeponywa. Na zaidi ya visa mia tatu vya makengeza, vikiponywa, chini ya muda wa miezi sita. Tulikuwa na rekodi yake. Shuhuda elfu arobaini kwa wagonjwa, kufikia sasa, za uponyaji, mashahidi, zilizotiwa sahihi na madaktari, na kadhalika.

68 Saa imewadia, enyi watu. Wakati umewadia. Ninasema hivi, nawe unaweza kuniita mlokole, ukitaka. Ninaamini kwamba hii inaonyesha Kuja kwa pili kwa Yesu Kristo. Amina. Kwa maana, kutakuwa na ishara na maajabu. Na jambo ni kwamba, kama huko katika Ufalme wa Mungu, jipenyeze ndani Yake. Hakika ningekuwa na ujuzi fulani wa kile ninachozungumzia, la sivyo Mungu hatawahi kuheshimu maombi yangu kufanya kile anachofanya. Na wewe uliye nje ya Ufalme, mtafute Kristo kama kimbilio lako sasa, wakati ukiweko na wakati una nafasi.

69 Kamwe sitasahau kauli fulani. Wakati mmoja nilikuwa nimesimama kwenye. . .

70 Isitoshe, kumaliza kuwasimulieni juu ya msichana mdogo huko Fort Wayne. Bibi Bosworth alimwambia, akasema, "Kipenzi. . . " Alikuwa akiuza vitabu, nyuma ya jengo.

71 Alitoka pale, akilia, akasema, "Bibi Bosworth," huyo ni mke wa Ndugu Bosworth, akasema, "Niliwaona wale watu wote wenye makengeza wakiponywa," alikuwa mwanamke kijana, kama miaka kumi na nane, makengeza mabaya kabisa. Akasema, "Ikiwa utaninii. . . " Kasema, "Laiti ningaliweza tu kuingia mle na kuingia kwenye mstari huo wa maombi! Lakini siwezi hata kupata kadi."

72 Bibi Bosworth, kwa huruma, akatoka kwenda kwa mtoto huyo. Akasema, "Mpenzi, kama utarudi moja kwa moja pale ambapo unaweza kumwona, na kweli. . . Usi—usifikirie tu sasa. Lakini amini kwa moyo wako wote kwamba hiyo ni karama ya Mungu, nitakuhakikishia atakuita baada ya dakika chache."

73 Nilikuwa nikiwaombea wagonjwa jukwaani, nilikuwa nimeuelekeza mgongo wangu kwa msichana huyo. Mara moja, nilihisi hilo likiingia, imani ikisonga. Nilitazama huku na huku, sikuweza kuibaini, kulikuwa na wengi waliosimama tu wakiwa wamesongamana. Nami nilijua ilikuwa inatoka kule, nami nikajaribu kutambua ilikuwa ni roho ya namna gani. Unaona, imani yake ilikuwa imepanda katika kiwango hicho.

74 Na nilipogeuka, hatimaye nikampata. Loo, umbali mara mbili ya jengo hili, nikaona ambapo alikuwa. Alikuwa amevaa koti la kijani kibichi. Nikasema, "Huyo msichana aliyesimama huko nyuma, ukiwa na makengeza, na koti la kijani kibichi, usiogope tena. Mungu amekuponya." Macho yake yakarudi kawaida kabisa. Hiyo ni moja tu ya maelfu ya visa vilivyotokea kwa njia hiyo.

75 Sasa wakati, kama tunaweza kufanya mkutano, kama ninyi watu mnaweza kukusanyika pamoja na kutupa tu kile unachofikiri *ni hiki, kile,* kukitupilia tu mbali. Usije kutazama tu. Njoo ukiamini na uone kama mambo yale yale hayatukii papa hapa jengoni.

76 Mara ya kwanza, nilipokutana na Dk. Bosworth, hapa, ilikuwa huko Miami. Tulikuwa na mkutano. Dk. Bosworth, anayejulikana kimataifa, uzoefu wa miaka arobaini katika kufundisha uponyaji wa Kiungu. Alifikiri kwamba siku moja Mungu angetuma ka—karama kwa kanisa. Ndipo aliposikia nilikuwa pale chini, aliwazia tu, "Vema, hiyo hapo tena, mtu fulani tu anayehubiri uponyaji wa Kiungu." Alikuja kwenye mkutano usiku mmoja. Na kupitia mkutano. . .Tulikuwa na, kile wanachokiita, mstari wa haraka; maelfu walikuwa wamesimama.

77 Alasiri hiyo, wavulana wawili wadogo kwenye WBAY, kituo cha utangazaji, walihojiwa, walizaliwa vipofu. Wote wawili walikuwa na macho yao, nao walikuwa nayo kule chini kwenye kituo cha utangazaji, wakihoji.

78 Kwa hiyo Ndugu Bosworth akatoka kwenye mkutano. Na ikawa kwamba, wakati mstari wa kufunga ulipoanza, kulikuwa na maelfu kadhaa ya kupita kwa usiku huo; hakuna kitu ila kuwawekea tu mikono wakipita, wanne sambamba.

79 Walimsukuma msichana mdogo. Sitamsahau mtoto huyo. Alikuwa mtoto mdogo mrembo. Alikuwa msichana mdogo, mwenye nywele za rangi ya shaba; jino moja mbele; na alikuwa na kishikizo kidogo kipya katika nywele zake, ama mnavyoviita vitu hivyo ambavyo wanawake huweka kwenye nywele zao. Wakamsukuma. . .Alikuwa katika magango, chini juu ya ki—kiuno chake kidogo hapa. Nao wangemsukuma kupitia mstari, nami nikamwekea mikono. Angetoka jukwaani, nao wangemrudisha kwenye mstari. Mbona, maskini mtoto huyo! Naye akaendelea kupita. Na ndipo mtu fulani angempitisha, nao wakamwekea mikono. Na alipokuwa akipita tena, akatazama juu, moja ya namna hizo za matabasamu madogo, unajua, na jino hilo limetokeza.

Na kitu fulani kikasema, "Msimamishe mtoto huyo."

80 Nikasema, "Kipenzi. . ." Niliona hakuwa na imani ya kuponywa wakati huo.

81 Lakini, unaona, hiyo ndiyo kazi ya karama. Hapa jukwaani, unaona jinsi Yeye, wakati mwingine, inakubidi kufanya kazi. Watu wanasema, "Loo, ninaamini, Ndugu Branham." Lakini hawa hapa, *hapa* chini; na hapa ndipo wanapopaswa kuwa, *hapa* juu. Vema, basi mambo yale ya kuwaambia magonjwa yao na siri za mioyo yao, imani huinuka mpaka nimfanye mtu huyo kuniamini.

82 Ndivyo Yeye alivyosema, "Ukiwafanya watu wakuamini, na uwe mwaminifu unapoomba, hakuna pepo anayeweza kushikilia hapo, basi." Inabidi amjue Bwana. Kisha . . . Na ninajua Yeye aliniambia jambo hilo.

83 Na ninapoweza kumfikisha mgonjwa huyo mahali mpaka imani yake ifikie jambo hili, hiyo ndiyo inanipa imani kamilifu. Sijawahi kuona ikishindwa. Na haitashindwa kamwe. Haiwezi kushindwa.

84 Ndipo yule msichana, walipomsukuma akapita, nikasema, "Kipenzi, simama moja kwa moja nyuma yangu." Naye akasimama kule nyuma, akiwa amemshika tu, akashikilia mkia wa koti langu. Nikasema, "Unaomba, mpenzi." Naye angeinamisha kichwa chake kidogo, akiomba.

85 Naye Ndugu Bosworth alikuwa ameketi, akiingiza haya yote, angali ana shaka kidogo. Naye alikuwa akiangalia, maana alikuwa huko nje, akitazama tu mwisho wa mkutano ukiendelea. Naye alikuwa . . . Ilikuwa usiku wa mwisho, naamini ulikuwa.

86 Naye alikuwa ameshikilia koti langu, nami niliendelea tu kuomba. Nilikuwa nimesahau kuhusu mtoto huyo. Nikageuka tena, nikasema, "Mpenzi, endelea kuomba," namna hiyo.

87 Na baada ya kitambo kidogo, nikaanza kuhisi imani hiyo ikianza kuingia, kama pigo la moyo, puh, puh, puh. Na ilipoanza . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kuenda namna hiyo, nikamgeukia. Nikasema, "Sasa, mpenzi," nami nikaweka mikono yangu juu yake na kumwomba Bwana Yesu.

Nikamwambia mama, nikasema, "Sasa mwondolee magango." Alisema, "Lakini, Ndugu Branham, nakuambia, yeye . . . "

88 Nikasema, "Usitilie hilo shaka, mama. Fanya kile unachoambiwa ufanye." Akasogea pale na kumwondolea magango mtoto huyo.

89 Huyu hapa anarudi chini na kushikilia hayo magango makubwa mno, kwa watu hao namna hiyo; mzima kabisa, mzima tu awezavyo kuwa, hiyo miguu midogo. Hiyo ni kweli, Dk. Bosworth? [Ndugu Bosworth anasema, "Amina."—Mh.] Na kuendelea na mkutano. Dakika chache tu, nilishikilia . . .

90 Loo, umbali maradufu, ama labda zaidi, wa jengo hili, chini ya hema kubwa la sarakasi ambapo watu walikuwa

wamesimama, nyuma kabisa kwenye barabara kuu, huko kwenye Bustani ya Princess. Kisha nyuma, nilishikilia . . .

91 Nilihisi kuna kitu kikiingia, kinaanza tena, "hwi, hwi." Nilijua ilikuwa ni imani. Sikuweza kujua ilikuwa inatoka wapi. Nikaendelea kugeuka, nikitazama; bali watu wakipita upesi sana, na hao wanalia, wakijaribu kukugusa na kadhalika.

92 Baada ya muda kidogo, nikaliona, kule nyuma kuelekea nyuma, jamaa mmoja aliyevaa shati jeupe. Nilisubiri, nijue ni roho ya aina gani ilimfunga. Mtu huyo alikuwa mlemavu. Alikuwa ameanguka kutoka kwa farasi, miaka michache kabla ya hapo. Alikuwa mfanyabiashara huko Miami. Mkono wake ulikuwa umelemaa, na mkono wake, namna *hiyo*. Alishuka kama mkosoaji, kukosoa katika mkutano. Na ndipo akaanza kupata imani.

93 Nilisimama na kusema, "Bwana, wewe hapo nyuma, wa nne kutoka kwenye safu, kurudi nyuma *huku*, uliyevaa shati jeupe, simama kwa miguu yako. Yesu Kristo amekuponya." Na aliposimama, mikono yake iliinuka. Maskini mke wake aliyejipaka rangi, ungefikiri alikuwa mtakatifu anayejifingirisha, kama maskini yule ndugu alivyosema asubuhi ya leo kwenye matangazo yake, kumsikia akipiga mayowe. Huyo hapo, amefunguliwa kikamilifu.

94 Ndugu Bosworth alichunguza kesi hiyo, kisha akaja kwangu. Alimwuliza mtu huyo yote kuhusu hilo. Naye alipokuja kuipata hivi, akasema, akaniuliza, akasema, "Ulijuaje kuwa huyo ndiye mtu huyo?"

95 Nikasema, "Bwana, naanza kudhoofika. Nilijua ilikuwa inatoka mahali fulani."

96 Naye akasema, akafika kwenye kipaza sauti, akasema, "Hilo linathibitisha Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Inathibitisha." Kasema, "Sasa, karama iliyokuwa ndani ya Yesu Kristo ingekuwa kama bahari hii yote nje hapa, ikipigapiga ukingoni. Karama ndani ya ndugu yetu itakuwa kama kijiko cha maji kilichotolewa ndani yake. Lakini kemikali zile zile zingekuwa kwenye kijiko hicho cha maji, kemikali za aina ile ile ambazo ziko katika bahari nzima." Hiyo ni kweli.

97 Na ni—ningeweza kujihisi nikizidi kudhoofika. Na hapo alikuwepo mtu huyo aliyefunguliwa kikamilifu.

98 Sasa hiyo imetukia mara mamia. Na kuna watu katika jengo hili, naamini, ambao wamekuwa kwenye mikutano mingine, kuishuhudia. Je, nina marafiki hapa ndani ambao wamekuwa kwenye mikutano mingine, wangeweza kushuhudia na kusema hiyo ni kweli? Inueni mikono yenu ikiwa mko hapa. Sasa mnaweza kuona. Biblia ilisema, "Kwa kinywa cha mashahidi wawili au zaidi."

99 Sasa, wakati, unaweza kuwa na jambo lile lile hapa Louisville. Hakuna haja ya mtu yeyote kuondoka hapa bila kufunguliwa kikamilifu. Huenda nisiwe na wakati tu kwa kila mtu kwenye jukwaa, lakini kila mtu anaweza kunufaika kwa hilo. Kama Mungu anaweza kujithibitisha Mwenyewe hapa kuwa ni Mungu, na kile ambacho kimethibitisha yale niliyosema kuwa ni kweli, basi mwaminini Mungu. Basi weka imani yako katika matendo, na uifanye imani yako kuwa ni tendo lililo hai, na Mungu atakwenda kukufanyia kazi papo hapo, na kukuponya.

100 Hot Springs, sasa, ilikuwa. . . Ninaamini ilikuwa huko Little Rock. Usiku mmoja magari ya kuchukulia wagonjwa yalikuwa yamesongamana sana, hata yakafungia magari ya mitaani. Ilibidi walete polisi pale ili kuwafanya waondoke kwenye kona, chini tu ya ngome huko Hot. . . katika Rock. . . Little Rock, Arkansas.

101 Kasisi Bw. Brown alikuwa mmoja wa wachungaji pale. Ukitaka kupata ushuhuda huu, mwandikie Kasisi G. H. Brown, 505 Victory Street, Little Rock, Arkansas, na usikilize hili. Nena kuhusu nguvu za pepo! Na ninii tu. . . Huo ulikuwa karibu mkutano wangu wa nne au wa tano, karibu yapata saa tano; mkono wangu ulikuwa umekufa ganzi kabisa.

102 Wakati mwingine ninapoenda nyumbani, mkono wangu unakufa ganzi kabisa, kabisa, hata inanibidi kuumiminia maji ya moto kwa karibu nusu saa, kupata hisia kuurudia tena, kutoka kwa ya kimwili. Na kuna saa; ninashika mikono ya mwanadamu, nikiwa na hiyo pale, itaisimamisha saa hiyo kabisa. Nina saa ya Longines sasa, ndiyo kwanza itoke kiwandani. Nikaishika. Ni mwitikio wa kimwili jinsi gani, au ni kitu gani cha kimitambo kinafanyia, sijui.

103 Lakini Bw. Brown alisema, "Njoo kwenye orofa ya chini, Ndugu Branham, kwenye jumba la mikutano." Akasema, "Nina kisa hapa chini ambacho hujawahi kuona chochote kama hicho." Vema, nilishuka nilipokuwa nikipumzika.

104 Nimeona tamasha za kutisha, lakini sijawahi kuona kitu kama hicho. Nimeingia kwenye hospitali ambapo wanawake vijana walitumia maliwato ya kitandani, kujipaka usoni, kichaa. Nimeona mambo ya kutisha, lakini kamwe sijaona chochote kama hiki. Akiwa amelala sakafuni alikuwa mwanamke wa karibu miaka thelathini, thelathini na tano, mwanamke aliyeonekana mwenye nguvu. Na mi—miguu yake ilikuwa imechomoza juu *hivi,* nayo ilikuwa inatokwa damu.

105 Kulikuwa na mtu aliyesimama kwenye ngazi, ndugu mzuri tu wa Arkansas akiwa amevaa ovaroli, na shati la samawati. Na, marafiki, nitasema, wakati mwingine mioyo iliyo bora zaidi hupiga chini ya hilo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, ninaamini. Si—sipendi maigizo yoyote. Ni—ninapenda wanaume na wanawake

wa mtindo wa kale, hiyo ni kweli; waliokolewa na Mungu, wakazaliwa mara ya pili. Naye alikuwa amesimama hapo, amevaa nguo zake kuukuu zilizoonekana chakavu. Nikasema . . . Akashuka.

Nikasema, "U hali gani?"

Naye akasema, "Habari za jioni. Wewe ni Ndugu Branham?" Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Nilifikiri ulikuwa."

106 Mfumo wa PA ulikuwa unaishusha huko pia. Walikuwa na kundi la wendawazimu upande mmoja.

107 Lakini hawangeweza kumzuia mwanamke huyu si kwa yeyote. Ilihitaji wanaume wapatao wanane au kumi kumleta ndani. Hawangeweza kumleta kwenye gari la kuchukulia wagonjwa. Hawangemwingiza kwenye gari la kuchukulia wagonjwa. Nao wakamtuma mtu kule kwenye gari, naye akapiga teke vioo vyote kutoka kwenye gari, na hao wanaume wakijaribu kumshikilia ndani ya gari. Naye huyo hapo, amelala chali. Daktari alikuwa amemdunga sindano kadha. Mabadiliko yake ya mapema ya maisha yalikuwa yamempeleka katika hili. Naye huyo hapo, amelala chali.

108 Nami nikasema, "Vema, nitatoka na kuona ikiwa ninahisi mitetemo yoyote."

109 Akasema, "Ndugu Branham, usitoke huko nje." Kasema, "Atakuua."

Nikasema, "Loo, sidhani," hivyo tu.

110 Nami nikatoka nje. Alikuwa amelala pale, akinitazama, kwa namna fulani akipepesa macho yake, akitazama. Nami nikasema, "Habari za jioni." Hakusema hata neno moja. Nikamshika mkono. Nikasema, "Habari za jioni."

111 Akasema, "Hata hajui jina lake mwenyewe, Ndugu Branham. Hajajua kwa miaka miwili."

112 Nami nikamshika mkono. Na kwa baraka za Mungu tu nikatokea kuwa mlinzi. Akanivuta kwa nguvu kwa mikono miwili, namna *hiyo*, na pengine angeivunja mifupa ya mwili wangu. Nami nikatupa mguu wangu nje na kumshika kifuani moja kwa moja. Alinivuta tu chini. Nikajiondoa kwake. Ndipo nilipokimbia kutoka kwake, ili kupanda ngazi, niliona kitu ambacho sijawahi kuona hapo awali. Mwanamke huyo, akiwa ameinua mikono yake miwili hewani, namna *hii*, alikuja akinifukuza, mgongoni mwake, kama nyoka. Ungeweza kumsikia akitambaa namna hiyo, sakafuni.

113 Sasa, huyo ni shetani. Unaweza kusema juu yake, kile unachotamani, lakini mwanamke huyo alikuwa amefungwa na shetani. Alinijia kwa mgongo wake, kama nyoka, naye akainuka pale na akagonga ubavu wa sakafu namna *hiyo*. Aligeuka,

akaweka miguu yake mikubwa yenye nguvu juu. . .akarusha teke *hivyo*. Kulikuwa na benchi pale. Aliipiga kwa kichwa chake; damu iliruka kutoka upande wa kichwa chake. Na—na akagonga kipande chake kikatoka. Naye akaikamata mkononi mwake, akamrushia mumewe na kupiga ukuta. Na plasta ikaanguka kutoka kwa ukuta, ambapo aliupiga kwa ninii ya kutisha sana. . .Mwendawazimu; mara ishirini nguvu zake, pengine. Na hapo hiyo ninii kuu. . .Alikuwa mwanamke mkubwa, mwenye nguvu, hata hivyo.

114 Na kisha akaanza kutoa sauti ya ajabu, akifanya, "E-e-e-e-e-e, eeeee," namna hiyo. Nilimtazama, nami nikawaza, "Mbona, sijawahi kuona chochote. . .Mungu amrehemu binadamu maskini aliyefungwa namna hiyo!"

115 Na mtu huyo akaanza kulia. Akasogea na kuweka mikono yake pande zote, akanikumbatia kwa mikono yake, kasema, "Ndugu Branham, sasa unasema hakuna mtetemo?" Akasema, "Na sijui nitafanya nini." Alilemewa kabisa, akaanza kulia. Akasema, "Anao watoto wadogo watano nyumbani." Tena akasema, "Mimi—mimi. . .Amekuwa mwanamke mzuri." Akasema, "Alipiga haro maskini mabonge haya na kunisaidia kupanda mazao ya pamba." Na akasema, "Alipoanza kuwa mgonjwa," akasema, "Nimefanya kila nilichoweza kufanya. Ni—niliuza shamba langu." Tena akasema, "Ili kumleta hapa, Ndugu Branham, nilikuwa na kitu kimoja kilichosalia, jozi ya nyumbu. Nami nikawauza, kumfanya ndugu huyo amlete maili mia mbili, kumleta hapa. Na sasa amepiga teke vioo kutoka kwenye gari, ndiyo sababu miguu yake inatoka damu." Akasema, "Hajaacha kuenenda kwa mgongo wake miaka miwili, na hata hajui jina lake mwenyewe."

Nikasema, "Vema, ndugu, hakika, Mungu anaweza kumponya."

116 Na karibu wakati huo aligeuka. Akasema, "William Branham, huna uhusiano wowote nami. Nimemleta hapa."

Akasema, "Kwa nini. . . "

117 Nikasema, "Huyo si yeye. Huyo ni yule ibilisi anayezungumza kutoka kwake." Hiyo ni kweli. Wanatambua. Wanajua.

118 Akasema, "Mbona, Ndugu Branham, hilo ndilo neno la kwanza alilonena katika miaka miwili."

119 Nikasema, "Ibilisi anatumia midomo yake tu, kama yule kwenye kisa cha jeshi."

120 Alikuja akitambaa kwa njia hiyo kwangu, akasema, "Huna uhusiano wowote nami." Akitambaa namna hiyo.

121 Nikasema, "Ndugu, unaamini kisa ulichosikia nikisimulia kuhusu ujio wa yule Malaika?"

122 Akasema, "Kwa moyo wangu wote," akasema, huku akinikumbatia kwa mikono yake.

123 Nilitembea hadi kwenye hatua ya kona, na nikaomba kwa moyo wangu wote, kwa Bwana Yesu. Nikasema, "Mungu, mwangalie maskini yule mwanamke; watoto wadogo watano wasio na hatia nyumbani, hakuna mama, mtoto mmoja anayenyonya." Nikasema, "Ni nini kinachoweza kutokea? Ee Mungu, turehemu!" Na Roho wa Bwana akaja. Na nikamwambia shetani amwache yule mwanamke.

Nikageuka nyuma, nikasema, "Sasa unaamini?"

124 Akasema, "Kwa moyo wangu wote. Nifanye nini naye Ndugu Branham?"

125 Nikasema, "Mrudishe. Mrudishe moja kwa moja kwenye sanatoriamu." Nikasema, "Kama hutatilia shaka hata jambo moja ambalo nimekuambia, tazama kitakachotokea."

126 Miezi miwili baadaye, nilikuwa huko Jonesboro, Arkansas, huko ambako mambo mengi yalikuwa yakitukia. Watu wapatao ishirini na nane elfu walikuwa wamekusanyika mjini. Nami nilikuwa nikizungumza, nami nikaona, wakinifinyilia ama kunipungia mikono yao, mwanamke fulani. Akasema, "Je, hunitambui, Ndugu Branham?"

127 Nikasema, "Hapana, mama." Alikuwa ameketi namna hiyo, na kila mtu . . .

128 Akasema, "Mimi . . . Ninyi nyote, nyote mniwie radhi." Akasema, "Nilitaka tu kukuona."

129 Ndipo nikamwona mtu fulani akicheka; ilikuwa ni mume wake. Naye huyo alikuwa ameketi hapo, mzima kabisa na akiwa na akili timamu, pamoja na watoto wake wadogo watano, mzima tu awezavyo kuwa.

130 Walikuwa wamemrudisha. Hakuwahi kulipiga gari teke hata mara moja, wakirudi. Walimrudisha kwenye seli iliyofungwa. Asubuhi ya pili, wakaingia kumlisha, naye alikuwa akijiandaa. Na katika asubuhi ya nne, tatu au nne, walimtoa kama mtu mzima, na kumpeleka nyumbani kwa watoto wake. "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

131 Angalia, rafiki, mapepo yanatambua Nguvu za Mungu wakati mwingine kabla ya wahudumu kuzitambua, na Wakristo. Je, ulijua hilo? Mara nyingi. Soma Biblia.

Kasisi aliposema, "Loo, Yeye ni Beelzebuli."

132 Ibilisi alisema, "Tunajua Wewe ni Nani, Mwana wa Mungu, Mtakatifu wa Israeli." Je, hiyo ni kweli?

133 Mnakumbuka wakati Paulo na Sila, wahudumu waliposema walikuwa wadanganyifu? Maskini yule mpiga ramli alisema walikuwa watu wa Mungu, waliokuwa na njia ya Uzima.

134 Kama sijakosea, Kasisi Hooper, kutoka Phoenix, Arizona, aliyeketi nyuma ya jengo, angeweza kuthibitisha tamshi hilo. Je, hukuwepo usiku huo, Kasisi Hooper? Kuna mtu alikuwepo pale ilipotukia. Mwandikie Kasisi G. H. Brown, 505 Victory Street, Little Rock, Arkansas, na umwulize akupe ushuhuda. Mwache akutumie. . .Hebu sanatoriamu ishuhudie hilo. Hiyo ni moja kati ya maelfu.

135 Mara moja tu zaidi. Siku iliyofuata, Malaika wa Bwana akaingia ndani ya jengo hilo. . .Na kisha nitaanzisha mstari wa maombi.

136 Nilikuwa—nilikuwa chini ya El Dorado. Ninapaswa kuwa huko kwenye uwanja wa mashindano yapata siku mbili usiku; mara tu ninapoondoka hapa, ninaenda Shreveport, halafu El Dorado, na kuendelea. Ni—nilikuwa kwenye kanisa dogo. Walisema, "Kama utakuja kuzungumza katika kanisa hili. . . "

137 Maelfu walikuwa wamejazana mjini. Na mwandishi alikuwa ameongoka; kwenye picha hii, mlinzi wa ho—hoteli; zote mbili kwa wakati mmoja. Walitaka kujua jinsi ya kumpata Yesu. Wamekuwa washiriki wa makanisa kwa miaka mingi; bali walipoona kazi ya Mungu, ambayo Mungu alikuwa akifanya nayo, katikati ya watu Wake. Walikuwa nami katika chu—chu—chumba kidogo. Nami nilikuwa nikihubiri.

138 Basi nilipotoka, kulikuwa na watu wanne wamekusanyika kunizunguka, wakaanza kutoka mlangoni. Na kusimama kwenye mvua huko nje, turubai ikiwa imewafunika wapendwa wao na kila kitu, kwa viunga vya jiji, watu wanaosubiri; hakuna mahali pa kwenda, la, hata nisingeweza kuingia, mahali popote, hakuna nyumba za kibinafsi. Walikuwa na magazeti yakiwa yametandazwa, turubai ya kushikilia, wakati mvua ya manyunyu ingenyesha, watoto wadogo walemavu, na kungojea zamu yao ya kujaribu kuingia kwenye mstari wa maombi. Ninakuambia, ndugu, hao ni watu wanaompenda Mungu. Hiyo ni kweli. Sitasahau kamwe. Mambo mengi ya ajabu, mafumbo yametokea, kwenye mstari. Nilianza kutoka nje ya jengo, watu wakilia, wakisukuma, wakijaribu kufika pale alipokuwa, namna hiyo. Walikuwa na mstari huu ukielekea kwenye gari.

139 Niliendelea kusikia mtu akipiga kelele, "Rehema! Rehema! Rehema!"

140 Nami nikatazama pande zote. Niliweza kuisikia mahali fulani, ilionekana kama kitu fulani kinaruka tu moyoni mwangu. Niliangalia. Ikisimama upande mmoja. . .Katika Arkansas wanayo she—sheria, watu weusi na wazungu hawawezi kuwa pamoja. Akisimama upande mmoja alikuwa ni mwanamume mweusi, ameshika kofia ndogo tu mikononi mwake, amesimama pale kwenye mvua, na mvua ikimpiga usoni. Mke wake akipiga mayowe, "Rehema! Rehema! Rehema!"

141 Niliwaza kuhusu maskini Bartimayo kipofu. Nami nikaanza kuendelea, na ilionekana kama Kitu fulani kiliniambia tu nisifanye hivyo. Mamia yao, wakisukumana. Nikasema, “Ninataka kwenda kule aliko yule mtu mweusi.”

142 Wakasema, “Ndugu Branham, huwezi kufanya hivyo.” Wawili kati yao walikuwa polisi. Wakasema, “Utaanzisha ghasia za kimbari sasa hivi.” Kasema, “Huwezi kufanya hivyo.”

Nikasema, “Lakini Bwana ananiambia niende pale alipo.”

143 Nami nilitokea tu upande mmoja na kwenda kule. Walitengeneza mviringo kidogo. Nami nikamsikia akisema, nilipokuja; bikizee, alisema, “Huyu hapa kasisi anakuja, mpenzi.” Jamani, jamani! Nikasogea karibu kidogo na pale alipokuwa.

Akasema, “Je, huyu ni wewe, Kasisi Branham?”

Nami nikasema, “Naam, bwana.”

144 Akaanza kunigusa usoni, kwa mkono wake. Naye akasema, “Kasisi, una dakika moja tu ya kusikia hadithi yangu?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

145 Akasema, “Kasisi,” akasema, “mama yangu mzee alikuwa mwanamke mzuri wa kidini.” Kasema, “Hakuwahi kuniambia uwongo katika maisha yake yote.” Akasema, “Amekufa sasa kama miaka kumi.” Akasema, “Sijawahi kusikia habari zako katika maisha yangu yote, hata.” Akasema, “Ninaishi kama maili mia moja kutoka hapa.” Kisha kasema, “Jana usiku. . . ” Akasema, “Nimekuwa kipofu sasa kwa miaka mingi.” Akasema, “Jana usiku, niliamka, na kando ya kitanda changu alisimama mama yangu mzee. Naye akasema, ‘Mpenzi, mtoto wangu, shuka hadi El Dorado, Arkansas, na ukaulizie mtu fulani kwa jina la Branham.’ Akasema, ‘Bwana ametoa karama ya uponyaji wa Kiungu. Utapata kuona kwako.’” Loo, jamani, nilijihisi kama moyo wangu ungekuwa mkubwa *hivyo*. Niliona Mungu alikuwa akinena.

146 Ikiwa mwanadamu hataliamini, Mungu atalitangaza kwa njia fulani kwa walio waaminifu moyoni. Atafanya hivyo.

147 Niliweka mikono yangu juu yake, na nikasema, “Ndugu, Bwana Yesu ambaye ametuma ono hili kwako amesimama hapa sasa kukuponya.” Nikaondoa mikono yangu kwake.

148 Nikamshika mkono; mtoto wa jicho alikuwa amekufa. Machozi yalimtoka na kudondoka shavuni mwake. Akasema, “Ninakushukuru Wewe, Bwana. Ninakushukuru Wewe, Bwana.”

Akasema, mke wake akasema, “Mpenzi, unaona?”

Akasema, “Ndiyo, naona.”

Kasema, “Loo, u—unaona kweli, mpenzi?”

149 Akasema, “Ndiyo.” Kasema, “Hilo ni gari jekundu lililoko hapo.” Loo, jamani! Alianza tu kupiga mayowe namna hiyo.

Na kisha wakanishika, wakatoka kuelekea kwenye gari.

150 Baadaye, nilishuka kwenye ndege karibu na Memphis, Tennessee, usiku mmoja. Nikaanza, nikasikia mtu akipiga kelele, “Halo, Kasisi Branham!” Nikaenda huko. Na alikuwa nani? Huyo hapo, mzima, angeweza kusoma Biblia yake ama chochote kile.

151 Nafikiri, “Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu, ambayo ingeokoa mnyonge . . . ”

152 Angali ni yeye yule usiku wa leo kama alivyokuwa wakati huo. Yuko hapa, marafiki. Jambo pekee ninalokuomba ufanye ni kuamini ya kwamba nimekuambia Kweli. Na uone Nguvu za Mwenyezi Mungu zikifanya kama nilivyosema. Zisipofanya, basi useme kwamba Ndugu Branham ni nabii wa uongo. Zikifanya, basi umwamini Mungu kwa ajili ya ushuhuda Wake.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

153 Baba yetu wa Mbinguni, loo, nafikiri, siku moja tutakaposhuka hadi mwisho wa safari, nami nije nyumbani Kwako, naomba ya kwamba utaniruhusu niingie, na ninaweza kupata kiti mahali fulani kule pamoja na watu hawa wapendwa wote ambao nimekutana nao. Tunaweza kuzungumza juu ya mambo, kumbukumbu tulizo nazo za mambo haya makuu ambayo Wewe umetufanyia. Na jinsi inavyopendeza, katika safari ya msafiri hapa, kukuona Wewe na kujua ya kwamba uko karibu, na Wewe uko hapa usiku wa leo kuwakomboa watu hawa wagonjwa na wanaoteseka.

154 Bwana, hadi wakati huu, hatujui ni nani uliyemchagua Wewe kuja katika mstari huu. Wewe wajua. Yupo mtu hapa. Wapo watu hamsini walio na kadi. Bwana, Wewe utatupatia. Unajua ni nani aliye hapa kuja. Nasi tunaikabidhi mikononi Mwako, Bwana.

155 Sasa bariki kila mtu. Na jalia wale, Bwana, ambao hawataweza kuwa katika mstari wa maombi, watakapowaona wengine wanaoumia na kuteseka, kama walivyo wao, wakiwaona wakifunguliwa, Ee Mungu, ninaomba ya kwamba imani yao itapanda na kuamini. Na, Ee Baba, jalia kwamba kutakuwa na uamsho wa mtindo wa kale utakaoanza tu katika jiji lote, Bwana, hata kila kanisa litakuwa na uamsho na watu waliopotea watakuwa wakiingia, wakimwamini Mwanao mpendwa. Tujalie, Mungu Mpendwa.

156 Sasa, Baba, Wewe wajua u—udhaifu wa mwanadamu. Na tunajua Nguvu za Mungu. Nami naomba ya kwamba utamtuma Malaika Wako, Yule ambaye alinitenga kutoka tumboni mwa mama yangu, kunileta katika maisha haya, na ameweka kwa kusudi hili, nitasimama hapa usiku wa leo. Mungu mpendwa,

kwa kusema neno hili kuu kwa ujasiri, mbele ya maelfu, na mamia ya maelfu ya watu, Wewe hujawahi kushindwa bado. Nami ninajua kwamba hutatupungukia usiku wa leo, lakini wewe utajalia usiku wa leo kwamba kila dhambi ya siri ya moyo itatajwa kwa watu; magonjwa yao wataambiwa, pepo wanaowafunga. Na kila mtu ataokolewa (sivyo, Baba?) kwa sababu tunakutumaini Wewe na kukupenda na kukuamini Wewe, na tunaomba haya kwa Jina Lako na kwa ajili ya utukufu Wako. Sikia maombi ya mtumishi Wako sasa, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

157 Vema, msimamizi wa mstari wa maombi sasa. [Ndugu mmoja anasema, "Nataka wale walio na kadi za maombi kuanzia B themanini na tano, hadi B mia moja, wasimame kwenye mstari kulingana na nambari yako upande wangu wa kulia, na kushoto kwako, kwenye ngazi za jukwaa. Kuanzia B themanini na tano, hadi B mia moja. Wengine wote wabaki wameketi."—Mh.]

158 Tunaweza kusema, wakati anapanga mistari, kila mtu hapa ndani anajua . . . Tunajaribu kusema hivi, kwamba lazima uwe na kicho. Hatutawajibika . . . Inanibidi niseme hivi kwa sheria, kila usiku. Siwajibikii wakosoaji wowote kwenye mkutano. Vitu hivi hutoka kwa mmoja hadi mwingine, hasa kifafa, na kadhalika namna hiyo. Nimeona watu wakija kwenye mkutano, wazima kabisa; naona mwenye kifafa ameketi hapa, na huyu mwenye kifafa anatoka akiwa mzima na mkosoaji anatoka akiwa kilema. Nimewaona wakiingia wengi kiasi cha ishirini na wanane kwa wakati mmoja, wakianguka kwa kifafa, sakafuni. Nguvu hizi za pepo zitapata mahali pa kwenda.

159 Na, marafiki, hiyo ni Biblia. Ni wangapi wanaojua hilo ni fundisho la Biblia, hebu tuone mkono wako. Hili ni kanisa la Agano Jipya likitenda kazi. Sivyo, marafiki? Nguvu za Mwenyezi Mungu za kukomboa.

160 Na wakati wanapanga watu, nadhani wale walio kwenye viti vya magurudumu, wangetaka tu mtulie, watakuja kukuchukua wakati wowote wao . . . Nambari yako ya kadi ikiwa tayari, wata—watakuita.

161 Sasa nataka kila mtu akumbuke hili. Mume—mumekaribishwa kila wakati kwenye mikutano, kila mmoja. Lakini ninapowauliza mwinamishe vichwa vyenu, lazima mwinamishe vichwa vyenu. Na kisha wakati mimi . . . usiinue kichwa chako mpaka unisikie nikisema kwenye maikrofoni hii, ama Ndugu Bosworth anayesimama hapa, kuinua kichwa chako. Ukiinua kabla ya hapo, sitawajibika kwa kile kinachotokea.

162 Bw. Hooper, akiwa ameketi karibu, alikuwa huko . . . Ninapenda kuona mtu hivyo, amekuwa kwenye mikutano mingine. Alikuwa Phoenix, Arizona, pamoja nasi, ambapo mmoja wa maofisa wa jiji hilo, ameketi kwenye mkutano.

163 Akasema, "Kweli, hiyo ni kesi nzuri ya saikolojia," kasema, "Nitaninii tu . . . Hakuna chochote kwake."

164 Niliendelea kumhisi mwanaume huyo. Alikuwa ameketi nyuma upande wangu wa kulia. Nikasema, "Mtu fulani upande wangu wa kulia, akiwa ameinua kichwa." Hakutaka kuinamisha kichwa chake.

Mmoja wa wahudumu akamwambia, akasema, "Inamisha kichwa chako."

Alikuwa ofisa wa mji, hivyo akasema, "Hainibidi kuinamisha."

Kwa hiyo, "Sawa."

Basi akanipa taarifa.

165 Nilikuwa na mtoto mdogo pale, naye alikuwa na pini ya nguo iliyozungushiwa kitambaa, kujaribu . . . Alikuwa na shambulio la kifafa; akawa na moja papo hapo kwenye jukwaa wakati huo. Wakati mwingine kifafa kinapokuja, huwatupa tu kwenye vipindi vya kifafa.

Nami nikasema, "Sawa, bwana, nilikuomba. Hayo ndiyo yote niwezayo kufanya."

166 Niliomba. Nikasema, "Mungu, usiruhusu mtoto huyu asiye na hatia ateseke kwa ajili ya mtoto huyo . . . kwa ajili ya mtu huyo, kutotii kwake." Kikamwacha mtoto huyo. Mwanamume huyo alitabasamu tu na kuendelea.

167 Takriban siku mbili baadaye, alikuja . . . akaanza kuwa na hisia za ajabuajabu, akasema, "Loo, ni mimi tu ninayefikiria hivyo, ni hayo tu." Kasema, "Ni ninii tu—ni mawazo yangu tu, yananisumbua." Alijaribu kujitikisa akiondokee.

168 Siku moja au zaidi baadaye, maofisa walimchukua mjini, wakizunguka huku na huko. Wiki sita hivi baadaye, alikuja . . .

169 Nilikuwa na ibada huko katika Charles Fuller . . . pamoja na Charles Fuller, kule Long Beach. Kama yeyote wenu alikuwepo, mnajua ni wangapi waliokuwa mle. Kulikuwa hasa na maelfu mle ndani, wakisimama juu-na-chini ufuoni, kwa hiyo wao . . . Hakuweza kuingia humo.

Alikwenda Los Angeles, asingeweza kuingia mle.

170 Na, hatimaye, Modesto. Mkewe, usiku wenye mvua, alianguka njiani. Ndevu zilikuwa zimeota usoni mwake, za kutisha, za kuchukiza. Naye huyo hapo. Kasema, "Ndugu Branham, jambo fulani halina budi kufanywa." Kasema, "Ha—ha—haninii, hata kula hali. Hatuwezi kummiminia maji ndani yake." Loo, alionekana wa kutisha. Ameketi pale, amekodoa tu macho.

171 Nikaingia ndani. Akaanza kufanya, "hummmm," akirudi nyuma kutoka kwangu, namna *hiyo*.

172 Nikawaambia wafunge mlango. Nasi tulikuwa tumechoka, tulikuwa tumekuwa kwenye jumba la klabu ya Jumamosi usiku pale, kwa saa nyingi, tukishughulika na wagonjwa. Niliwafanya Ndugu Brown na Ndugu Moore kufunga mlango, kuwazuia watu wasiingie. Mke wake alikuwa na matope kutokana na kuanguka njiani, na akashikilia miguu ya suruali yangu. Sikuweza hata kusogea. Hawangeweza kuniburuta, yeye akiwa ameshikilia, ili nimfikie mumewe.

173 Takriban dakika arobaini na tano baadaye, ilimwacha. Alinizungushia mikono yake na kunikumbatia. Akaweka kofia yake kichwani mwake namna hiyo, akanishika mkono, akaenda nyumbani kuwa mtu mwenye afya.

174 Nawaambieni, marafiki, ikiwa ningekuwa mkosoaji, hata nisingeketi karibu na kile kilichokuwa kinaendelea. Nipo hapa kukusaidia na sio kukuzuia. Vema, sasa, kumbuka hilo tu. Kama utaendelea kuinamisha kichwa chako, kama jambo fulani lingetokea, ninawajibikia hilo basi. Sasa, huwezi kusimulia juu yake, kwa sababu nitaijua utakapokuja hapa. Lakini sasa iweni na kicho tu, iweni katika maombi. Ninapokuomba uinamishe kichwa chako, endelea kuinamisha kichwa chako. Ulifanya jana usiku, vizuri sana. Basi fanya jambo lile lile usiku wa leo, kila kitu kitakuwa sawa. Hivi wewe. . .

Wekeni mistari yenu tayari.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa muda kidogo.

175 Baba, ninatambua kwamba huu ni wakati mzuri sana. Ni wakati ambapo tunasimama uso kwa uso na adui. Na hapa kuna vilema, wanaoteseka, na watu wanaokufa. Hapa kuna watu ambao wamesimama hapa kwenye mstari, ambao labda wana kansa au labda wana shida ya moyo. Sijui wana shida gani sasa. Lakini Wewe utamwambia mtumishi Wako. Nami nakuomba, Wewe, ya kwamba utamkomboa kila mmoja wao kikamilifu kabisa. Na jalia Shetani aitwe atoke kila wakati, na jalia afichuliwe mbele ya wasikilizaji. Jalia kila mtu awe mzuri, Bwana, anayeshirikiana, wote Mkristo. Na tuwe na mkutano mzuri usiku wa leo. Naomba Nguvu za Roho Mtakatifu zienee kote jengoni, ziponye kila mtu aliye ndani ya jengo hili, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Hebu tuimbe, mara moja tu, tafadhali.

> Amini tu. . .

Kila mtu kwa kicho tu uwezavyo kuwa.

> Mambo yote yawezekana, amini tu;
> Amini tu, amini tu,
> Mambo yote yawezekana, amini tu.

Sijui kama tunaweza kuimba hivi sasa:

> Sasa naamini. . .

176 Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? Inua mkono wako unapouimba.

. . . sasa naamini, (Bwana asifiwe!)

177 [Sehemu tupu kwenye kanda.—Mh.] . . . ana kansa au shida ya kike. Na kwa muda kidogo tu; yote mawili yaligonga karibu sawa. Ni shida ya kike, ndivyo ilivyo. Hiyo ni kweli? Naam. Hakika. Karibu ni kansa, hata hivyo, ndivyo ilivyo. Maisha hayajawa kitanda cha maua cha urahisi kwako, sivyo? Hapana. Ulikuwa na matatizo mengi . . .

50-0100 Magonjwa Na Mateso
Church Of The Open Door
Louisville, Kentucky Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org